MAONI & UCHAMBUZI

Nukuu

"Uongozi imara si utaalamu wa kutoa hotuba ama kupendwa, bali uongozi ni kutoa matokeo yanayotarajiwa."

Peter Drucker (1909-2005)

Viongozi tumieni vikao kutatua kasoro zenu

Mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda ametengua agizo la mkuu wa wilaya ya Ilala, Sofia Mjema la kupiga marufuku ibada zinazofanyika katikati ya wiki.

Sofia naye alifafanua agizo lake, akisema kwamba alimaanisha madhehebu yanayoanzishwa bila kufuata utaratibu na ambayo yanafanya ibada kwa sauti kubwa na hivyo kusababisha kero kwa wakazi walio jirani na nyumba hizo za ibada.

Tofauti hiyo baina ya viongozi wa mkoa mmoja ni sehemu tu matukio ya kutofautiana baina ya viongozi. Kuna mifano mingi ya kiongozi kutangaza agizo fulani na baadaye wa juu yake akajitokeza na kulifuta hadharani na kuacha wananchi wasielewe nini kimewakuta viongozi wao.

Tusingependa kuorodhesha mifano ya matukio hayo, lakini tuimeona ni muhimu kuchukua tukio hilo la Dar es Salaam kama mfano unaofaa kuzungumzia tofauti za viongozi ambazo wakati fulani huonyesha kuwa kuna udhaifu kwa anayekosolewa na anayekosoa.

Tunafahamu kiongozi anapaswa kuwa na stadi zote za uongozi ukiwamo uwezo wa kujenga umoja, kutatua changamoto, kutafuta maridhiano na kuheshimu miiko ya kazi.

Kilichotokea kati ya Makonda na Sofia ni mwendelezo wa tabia iliyoanza kuzoeleka kwa viongozi wa Serikali ya kuumbuana hadharani, hali ambayo haisaidii kujenga uongozi wa pamoja.

Utendaji katika ngazi yeyote ya uongozi unafanyika kwa kutumia vikao, hata kwenye familia baadhi ya maamuzi hufanywa katika vikao.

Katika siku za karibuni, viongozi hata wale wa kisiasa wameanza kujenga utamaduni mpya wa kuacha kutumia vikao kusemana, kukosoana, kuelekezana na kushambuliana na badala yake kutumia mtindo mpya wa kuumbuana hadharani.

Ifahamike kwamba heshima kwa viongozi huwa bora zaidi pale wanapoonyesha msimamo wa pamoja na uongozi wa pamoja mbele ya wananchi wanaowaongoza.

Hivyo, viongozi wanapokosoana hadharani wakati wa kutekeleza majukumu yao, huwafanya wananchi wachanganyikiwe na pia kuacha kumuheshimu aliyekosolewa.

Pia, hatari tunayoiona ni kwamba viongozi hawa wanajenga picha ya kudharauliwa na wananchi ambao watawaona kuwa hawana uongozi wa pamoja na hata utekelezaji wa maagizo yao kwa wananchi unaweza kuleta shaka.

Tunashauri viongozi wetu warudi kwenye misingi ya uongozi wa pamoja, wazungumze tofauti zao ndani ya vikao badala ya kuwaonyesha wananchi kwamba wao wenyewe hawapeani staha.

Hulka ya binadamu anapoona kiongozi anayemuheshimu akiumbuliwa hadharani na kiongozi mwingine wa juu, huanza kutokuwa na imani na kiongozi huyo na hatimaye kumdharau.

Mbali na dharau, utekelezaji wa miradi ya maendeleo unaweza ukazorota zaidi kwa kuwa kiongozi aliyeumbuliwa hadharani hatakuwa na nguvu ya kuhimiza jambo kwa wananchi.

Ni vema basi utaratibu wa kazi wa ama kuitana ofisini na kuzungumza kasoro zilizopo au kutumia vikao kurekebishana, kukosoana na kushauriana ukaendelezwa badala ya kila mmoja kufanyia kazi hadharani na kuwachanganya wananchi.

Tunaamini kama kuna kiongozi amekosea kutoa agizo, njia sahihi ni kuzungumza naye faragha na kumueleza makosa yake na hivyo kutafuta njia ya kurekebisha kosa lake bila ya kuwachanganya wananchi.

Ieleweke hoja yetu haimaanishi kuwa kiongozi anapofanya makosa yanayolalamikiwa na wananchi, asisemwe. La hasha. Tunachoshauri ni viongozi kufanya maamuzi ya pamoja na kuepusha maamuzi yanayoweza kusababisha wakatofautiana hadharani.

KIPANYA

HUTOLEWA NA MWANANCHI COMMUNICATIONS LTD

Barabara ya Mandela, SLP 19754, Dar es Salaam.
+255 22 24 50875, 0754 780647
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Francis Nanai: Mkurugenzi Mtendaji
Bakari Machumu: Mhariri Mtendaji Mkuu
Frank Sanga: Mkuu wa Kitengo cha Habari/ Mhariri

Ukifanya haya utadumu katika kazi yako

BENSON CHONYA

Upo msemi mmoja wa lugha yetu ya Kiswahili usemao "thamani ya kazi huonekana kwa mtu ambaye hana kazi".

Ukipata nafasi ya kutaka kujua ukweli kuhusu usemi huu, jaribu kumtafuta mtu ambaye hana kazi halafu muulize mikakati yake endapo utampa kazi fulani mtu huyo. Wengi watakupa majibu chanya yenye kukupa hamasa ya kutaka kumuajiri mtu huyo.

Lakini mtu huyo huyo atakapoanza kazi utashangaa ufanisi wake unashuka kwa kiwango cha juu sana kila siku.

Hali hiyo pia, inatukumbusha usemi usemao, 'kazi mbaya ukiwa nayo.' Ni wazi kuwa watu wengi ambao wamebahatika kupata kazi, huwa hawazithamini kazi zao na kusahau yake maneno waliyoyasema wakati hawana kazi kuwa, wakipata wataheshimu kazi na kufuata misingi yote anayoitaka bosi husika.

Hata hivyo, baada ya kupata kazi hali huwa tofauti na kushindwa kutimiza yanayohitajika.

Suala ya kushuka kwa ufanisi wa kiutendaji wa wafanyakazi ni mtambuka, wapo baadhi ya watu wanapopata ajira huwa hawadumu katika ajira hizo wengi huleta masihara ambayo hayana kichwa wala miguu.

Kwa hakika mambo hayo hayana msaada wala mchongo wowote katika kuleta matokeo chanya katika kazi.

Pia, wafanyakazi wengi wamejikuta wakibweteka kabisa katika kufanya kazi, mwisho wa siku waajiri wao wamekuwa wakiamua kuwafukuza kazi hizo husika na kutafuta watu wengine ambao watafaa.

Huenda hata wewe unayesoma makala haya umekuwa ukikumbwa na tatizo hili la kufukuzwa kazi mara kwa mara. Kama wewe ni miongoni mwa watu hao ambao wamekuwa wakifukuzwa katika ajira zao basi leo nimeona ni vyema nikusogezee machoni pako uchambuzi huu muhimu ambao utakusaidia kwa namna moja ama nyingine namna bora ambavyo utaweza kudumu katika ajira yako.

Ili uweze kudumu katika ajira yako inatakiwa kuzingatia mambo yafutayo.

Kwanza, fanya kazi kwa juhudi na bidii. Matokeo makubwa ya kitu chochote unachokifanya hutokana na juhudi zako katika kufanya kazi kwa juhudi zote. Ili uweze kudumu katika ajira yako unatakiwa kuelewa misingi ya kufanya kazi kwa bidii ili uzalishe kitu au huduma iliyo bora.

Ukifanya kazi kwa bidii na juhudi zako zote ni kwamba mwajiri atakupenda zaidi na hii ndiyo itakuwa siri yako ya kudumu katika ajira unayoifanya. Pia, zingatia suala la muda katika kazi; siri pekee itakayokufanya udumu katika ajira yako ni pamoja na kuelewa namna sahihi ya matumizi ya muda.

Kila wakati zingatia muda maalumu ambao ulikubaliana na mwajiri wako katika kuanza na kumaliza kufanya kazi.

Hakuna mwajiri hata mmoja katika sayari hii ya dunia ambaye atakuwa tayari kuona mfanyakazi wake anakuwa ni mtu wa kuchelewa kazini kila siku, kwa sababu lengo la mwajiri kukuajiri wewe ni pamoja na kuona unatumia muda vyema kama ambavyo mmekubaliana katika kufanya na kuzalisha vitu vyenye tija kwa wakati sahihi.

Ila endapo itatokea kinyume chake, hakuna mwajiri atakayekuwa tayari kuendelea kubebe watu wezembe wasio heshimu muda katika kazi yake.

Waajiri wengi wanapenda watu ambao wanafanya kazi kwa juhudi huku suala la muda katika kutenda kazi likichukua nafasi pia.

Faida ambayo utaipata endapo utaamua kufanya kazi kwa kushirikiana na wafanyakazi wengine ni kwamba utaweza kujifunza mambo mengine mapya ambayo ulikuwa huyajui.

Kuwa mtu wa kushikirikiana na wafanyakazi wengine; suala la kudumu katika ajira huendana na sambamba na suala la kushikiriana vyema na wafanyakazi wengine. Unapofanya kazi binafsi pasipo kushirikiana na wengine hata matokeo pia yatakuwa ni kidogo, tofauti na utakavyowashirikisha wengine.

Hata wahenga walituachia usemi mzuri usemao "umoja ni nguvu ila utengano ni dhaifu." Hivyo, kila wakati unapaswa kushirikiana na wafanyakazi wangine ili kuleta matokeo chanya katika kazi unayoifanya.

Pia, faida ambayo utaipata endapo utaamua kufanya kazi kwa kushirikiana na wafanyakazi wengine ni kwamba utaweza kujifunza mambo mengine mapya ambayo ulikuwa huyajui.

Ubinafsi na umimi katika kazi humfanya mtu ashindwe kaufanya kazi kwa ufanisi. Amua leo kufanya kazi kwa kushirikiana na watu wengine hiyo itakusaidia kulinda kazi unayoifanya na hatimaye utadumu katika kazi hiyo.

Mwandishi wa uchambuzi huu ni mtaalamu wa ujasiriamali anapatikana kwa namba 0757 909942